# MAELEZO YA MAJUKUMU YA ANAEJITOLEA

MKUTANO MKUU 2026

## MSAIDIZI WA KATIBU

Anayejitolea atamsaidia katibu wa Kamati ya kisheria na kurekodi mabadiliko ya maandishi kwenye hifadhidata kadri kila ombi linavyoshughulikiwa wakati wa kikao cha Kamati ya kisheria na Kipindi cha Mjadala. Watu nane watahitajika kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 1, mmoja kwa kila Kamati ya kisheria. Watu watatu wanaweza kuendelea hadi Septemba 5, wakibadilishana jukwaani kwa kila Kipindi cha Mjadala. Mahitaji maalum ni pamoja na ujuzi wa kutumia kompyuta na kibodi kwa kuingiza taarifa kwenye hifadhidata na umakini kwa undani. Wanaojitolea kumsaidia katibu ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

## UTHIBITISHAJI WA STAKABADHI

Wanaojitolea hawa watakuwepo katika vipindi vya mjadala wa kongamano kuthibitisha stakabadhi na kusimamia mabadiliko ya wajumbe mbadala. Wanaojitolea kuthibitisha stakabadhi ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

## HUDUMA YA MAPOKEZI

Wanaojitolea watakaribisha na kusaidia washiriki kabla, wakati na baada ya kongamano. Baadhi ya washirika wa kikundi watakuwepo uwanja wa ndege kwa ajili ya kuwakaribisha watu binafsi na kuwasaidia kufika kwenye usafiri wa kuelekea kwenye kongamano. Washirika wa kikundi watapatikana wakati wa kongamano kujibu maswali na kutoa maelekezo. Wale wanaohudumu katika ukumbi wa kongamano wanapaswa kufahamu taarifa zilizomo katika nyaraka muhimu (kama vile Jarida la Kongamano kabla ya Mkutano, ramani, ratiba, na Mpango wa Shirika na Agano la Maisha Yetu Pamoja) ili waweze kujibu maswali ya washiriki kwa haraka na kwa usahihi. Baada ya kongamano, baadhi ya washirika wa kikundi watapatikana kusaidia wale wanaohitaji msaada wakati wa kujisajili kwenye uwanja wa ndege. Kuwa na ujuzi wa lugha nyingi kama Kiingereza na lugha nyingine rasmi za kongamano (Kireno, Kihispania, Kifaransa, Kikorea, na/au Kiswahili) itakuwa faida kubwa. Wanaojitolea kuhudumu kama wakaribishaji lazima wafike kabla ya tarehe 26 Agosti. Wanaojitolea kwa timu ya mapokezi ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

## MKALIMANI

Wakati tafsiri ya akili mnemba haitumiki, wakalimani watahitajika kwa lugha rasmi sita za GMC (Kiingereza, Kikorea, Kifaransa, Kireno, Kihispania, na Kiswahili), lakini hasa Kiswahili kwenda Kiingereza wakati wa vipindi vya mjadala na vya Kamati ya kisheria. Wanao hudumu katika jukumu hili wanatarajiwa kuwepo kadri inavyohitajika. Wakalimani watarejeshewa gharama za usafiri, malazi, na chakula, pamoja na posho kidogo.

## WASIMAMIZI WALINZI

Kuhakikisha mazingira ya ukaribisho, usalama na amani kwa wote wanaohudhuria kongamano. Wasimamizi walinzi watakuwa na wajibu wa kudhibiti maeneo yote ya kuingia ikiwemo eneo la kupigia kura la wajumbe. Waombaji wa nafasi hii, tafadhali eleza kama una uzoefu au uthibitishaji katika ulinzi/usalama, usimamizi, uangalizi au CPR. Wanaojitolea wa timu ya wasimamizi walinzi ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

## USAIDIZI WA TIMU YA MISHENI

Timu ya misheni inapanga uzoefu wa misheni na uinjilisti nje ya eneo kuanzia Agosti 29 hadi Septemba 5. Wanaojitolea wanahitajika kusaidia kwenye mapokezi, usajili na kuwasaidia washiriki kila siku. Wanaojitolea kwa usaidizi wa timu ya misheni ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

## USAIDIZI WA OFISI

Kama mshirika wa timu ya usaidizi wa Ofisi unayejitolea, utasaidia kazi muhimu za usimamizi na ugavi ili kuhakikisha ufanisi wa Baraza kuu la Kanisa la Kimethodisti Ulimwenguni 2026. Jukumu hili la nyuma ya pazia husaidia wafanyakazi kupanga kongamano, wawakilishi na washiriki huku likisaidia kuweka mazingira yaliyopangwa, ya ukaribisho na yanayotia moyo wa kiroho. Wanaojitolea wa timu ya usaidizi wa Ofisi ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

# MAELEZO YA MAJUKUMU YA ANAEJITOLEA

MKUTANO MKUU 2026

## WAHUDUMU

Wafanyakazi muhimu wa mstari wa mbele wanaowawezesha wawakilishi kutambulika ili wazungumze, kutoa hoja, na kushughulikia changamoto za kimsingi za kiteknolojia. Wahudumu pia hufanya kazi ya uangalizi, kuhesabu kura, kusafirisha ujumbe, kuendesha shughuli ndogo ndani ya kituo cha kongamano, kuwasaidia wawakilishi wasiozungumza Kiingereza, kusambaza maandishi rasmi, kufanya majukumu ya ukusanyaji vifaa mwishoni mwa kongamano, na kufanya majukumu mengine kama itahitajika. Kuwa na ujuzi wa lugha nyingi kama Kiingereza na lugha nyingine rasmi za kongamano (Kireno, Kihispania, Kifaransa, Kikorea, na/au Kiswahili) itakuwa faida kubwa. Wanaojitolea kwa ukarani ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

## MBUNGE

Hufanya kazi kama mshauri kuhusu mchakato wa Wenyeviti wa Kamati za Kisheria na Maaskofu wanaoongoza, akiwasaidia wenyeviti na maaskofu kufuatilia mahali walipo kwenye mchakato wa hoja na marekebisho, nk. Husaidia kutengeneza mafunzo kuhusu taratibu za msingi za Bunge. Inapendekezwa uwe umepata mafunzo rasmi katika taratibu za Bunge, kama hujaidhinishwa kuwa Mbunge. Inahitaji mikutano miwili ya Zoom kufanyika wakati wa majira ya kiangazi. Hoteli, usafiri wa ndege na pesa za kujikimu kwa kila siku zitalipwa na GMC. Watawasili Johannesburg tarehe 27 Agosti. Baadhi ya wanaojitolea katika jukumu hili watahitajika kufanya kazi siku tatu za kwanza za kongamano pekee na wanaweza kurudi nyumbani tarehe 2 Septemba.

## KUNDI LA MAOMBI

Wanaojitolea wa Kundi la Maombi kwa Baraza Kuu wana viwango viwili vya ushiriki: 1) Kundi la maombi lililo kwenye eneo la tukio linajitolea kuhudumu kwa ratiba ya zamu katika chumba cha maombi wakati wote wa kongamano, na pia wanahudumu inapohitajika kujibu Wito wa madhabahu; na 2) kundi la maombi kwa Wito wa madhabahu, linalopatikana tu wakati wa huduma za ibada ili kuhudumia hasa wito wa madhabahu. Hii inaruhusu watu kushiriki katika fursa nyingine za kongamano kama vile, mwakilishi/mdabala, Uzoefu wa Utume. Wanaojitolea wote wa kundi la maombi wanatarajiwa kuhudhuria mafunzo ya ZOOM kabla ya kongamano. Maono ya chumba cha maombi ni kualika Uwepo wa Bwana katika mikutano yote ya kongamano na kutoa nafasi takatifu ambapo watu wanaweza kukutana na Bwana wakati wote wa kongamano. Mazungumzo kabla ya kongamano na mshirika wa Kamati ya maombi ya Baraza kuu yatasaidia kubainisha mahali bora pa kupangia waombaji wanaojitolea. Waombaji wanaozungumza lugha nyingi wanatiwa moyo sana kuomba! Wanaojitolea wa kundi la maombi ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea. Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli. Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5. Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.




# MAELEZO YA MAJUKUMU YA ANAEJITOLEA

MKUTANO MKUU 2026

## USAJILI

Wakague washiriki kabla ya kongamano na wagawie beji, mishipi ya shingo, na mikanda ya mikononi ya rangi. Aweze kutumia kompyuta kibao zilizotolewa kwa ajili ya michakato ya usajili. Baadhi ya washirika wa timu watakuwepo kongamano likiendelea ili kushughulikia masuala kama vile kubadilisha beji zilizopotea, kusaidia wawakilishi wakuu na uthibitisho wa mbadala. Kuwa na ujuzi wa lugha nyingi kama Kiingereza na lugha nyingine rasmi za kongamano (Kireno, Kihispania, Kifaransa, Kikorea, na/au Kiswahili) itakuwa faida kubwa. Lazima ufike kabla ya tarehe 26 Agosti na ukae hadi tarehe 30 Agosti.  Wanaojitolea wa usajili wanaweza kubadilika kutoka usajili kwenda mapokezi wakati wa kongamano. Wanaojitolea kwa timu ya usajili ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea.  Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli.  Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5.  Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.

## USAIDIZI WA KURA

Kusanidi na kusimamia programu ya mfumo wa kura kwa ajili ya matumizi katika vipindi vya mjadala. Hii inajumuisha kuandika hoja zitakazopigiwa kura kabla na wakati wa vipindi vya mjadala (hivyo ni lazima uwe na ujuzi wa kompyuta ikiwa ni pamoja na uandishi wa haraka na uingizaji wa data). Kusimamia usambazaji wa vifaa vya kupigia kura kwa kushirikiana na timu ya uthibitishaji wa stakabadhi, kushughulikia mabadiliko ya betri kati ya vipindi ikiwa itahitajika. Kuandaa mafunzo kwa wahudumu na wawakilishi kuhusu matumizi ya vifaa vya kupigia kura. Kutoa usaidizi kwa maswali ya kiteknolojia na changamoto kuhusu mfumo wa kura. Kufanya kazi vizuri kama timu na wengine. Wanaojitolea wa timu ya kura ni nafasi zisizolipwa. Gharama za nauli na usafiri ni wajibu wa mtu anayejitolea. Gharama za hoteli na chakula mjini Johannesburg zitalipwa na GMC.

## USAIDIZI WA UABUDU

Timu ya Usaidizi wa Uabudu inahakikisha utekelezaji mzuri wa huduma zote za ibada. Wajibu unajumuisha maandalizi ya jukwaa na madhabahu, kutayarisha vipengele vya meza takatifu, na kuratibu na Timu ya Uzalishaji kuwapa vifaa wazungumzaji na viongozi wa uabudu. Zaidi ya hayo, washirika waliobarikiwa na vipaji vya muziki wanaweza kusaidia huduma ya uabudu kwa kuimba kwenye kwaya ya Ufunguzi wa Ibada na labda kutoa muziki kwa ajili ya maombi na huduma za meza takatifu. Wanaojitolea wa timu ya usaidizi wa uabudu ni nafasi zisizolipwa. Gharama zote zinazohusiana na nauli ya ndege, hoteli na chakula ni wajibu wa mtu anayejitolea.  Kifungua kinywa kimejumuishwa katika hoteli.  Chakula cha mchana kitatolewa katika Kituo cha Mikutano cha Sandton kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 5.  Chakula cha jioni kitatolewa Sandton tarehe 30 Agosti, 31 Agosti na 2 Septemba.